

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU**

**08 MEI, 2019**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU – TAREHE 08 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

186. MHESHIMIWA MUNIRA MUSTAPHA KHATIB (VITI MAALUM):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Vyama vya Wafanyakazi nchini licha ya kuwa na uwezo wa kujitegemea bado vinaendelea kutoza ada kubwa ya Uanachama mathalan, Chama cha Walimu (CWT) kinatoza asilimia 2:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kulinda maslahi ya Watumishi kwa kuleta Sheria ya kupunguza makato hayo.

**187. MHESHIMIWA KITETO ZAWADI KOSHUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuelekeza Taasisi zote nchini kuwa sifa mojawapo ya kuajiriwa iwe ni umri wa mika 21 – 35 ili kuwezesha Vijana wengi wanaotoka vyuoni kupata ajira.



**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**188. MHESHIMIWA PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kuna uhaba mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi Wilayani Mwanga:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu 384 wanaohitajika.

**189. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe.

**WIZARA YA KILIMO:**

**190. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Tanzania ina ardhi kubwa yenye rutuba ya kutosha na inawezekana kabisa kulima mazao yasiyotumia mbolea za Viwanda ambayo bei zake ni kubwa sana katika Soko la Dunia:-

- (a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kutoa elimu hiyo kwa Wakulima;
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuona kuwa Tanzania ni nchi inayoongoza kwa kuzalisha mazao yasiyokuzwa kwa kutumia mbolea za Viwandani.

**191. MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI  
(VITI MAALUM)**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-  
Changamoto kubwa inayowafanya Wanawake  
wa Tanzania wasishiriki kwenye Sekta ya kilimo  
ni ufinyu wa Bajeti na mitaji kutoka kwenye  
Taasisi za Kifedha:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya ushiriki wa  
Wanawake kwenye Sekta ya Kilimo, ukizingatia  
changamoto hizo.

**WIZARA YA NISHATI:**

**192. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE  
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-  
Jimbo la Tunduru Kusini lina jumla ya Vijiji 65,  
kati ya hivyo ni Vijiji vinne tu ndiyo vimefikiwa na  
umeme wa REA Awamu ya I na II.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa REA  
katika Vijiji 61 vilivyobaki.

**193. MHESHIMIWA ESTER AMOS BULAYA (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- TANESCO Mkoa wa Mara katika zoezi la kupeleka umeme Vijijini, walipitisha nguzo za umeme kwenye maeneo ya Watu katika Kijiji cha Nyabeu Kata ya Guta na uthamini ulifanyika na iliahidi malipo kufanyika lakini hadi leo hawajalipwa na badala yake wanaambiwa maeneo hayo ni ya TANESCO:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawalipa Wananchi hao fidia stahiki;
- (b) Je, ni kwa nini TANESCO inamiliki maeneo kabla ya kulipa fidia.

**WIZARA YA MAJI:**

**194. MHESHIMIWA PETER AMBROSE LIJUALIKALI (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kwa nini Serikali isifute kodi kwenye vifaa vya kusambazia maji kutokana na matatizo ya maji tuliyonayo katika Taifa letu.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **195. MHESHIMIWA ASHA MSHIMBA JECHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Tanzania imebarikiwa kuwa na ukanda wa Bahari na Maziwa:-

Je, Wananchi wa maeneo hayo wameandaliwaje kufaidika na rasilimali zinazopatikana katika ukanda wa Bahari na Maziwa.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
08 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**